



KUWA SALAMA MTANDAONI



Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum
Mji wa Serikali - Mtumba,
Barabara ya Afya,
S.L.P 573,
40478 DODOMA.

Simu: +255 (26) 2963341/2963346

Fax: +255 (26) 29634348

Barua Pepe: ps@jamii.go.tz

Tovuti: www.jamii.go.tz

Oktoba 2022

MPENDWA MTOTO,

Bila shaka umewahi kusikia kuhusu mtandao. Uchunguzi uliofanyika kuhusu matumizi ya mtandao kwa watoto nchini Tanzania umeonesha kuwa, takriban asilimia 67% ya watoto waliopo kati ya umri wa miaka 12-17 hutumia mtandao.

Kupitia intaneti, watoto na watu wazima huweza kuwasiliana na mtu yeyote ndani na nje ya Tanzania, kutafuta taarifa, kutazama video na kufanya mambo mengine mengi. Ili kupata intaneti, unaweza kutumia simu ya mkononi, kompyuta ya mkononi, kompyuta ya mezani, kishkwambi, saa janja, runinga janja, na vifaa vingine. Naamini unafahamu vifaa vingi zaidi ya vilivyotajwa hapo juu.

Kwa bahati mbaya, matumizi ya mtandao yanaweza pia kukuunganisha na watu unaowajua na usiowajua ambao hawana nia njema. Hivyo, kupitia mtandao unaweza ukawa kwenye hatari ukiwasiliana na watu ambao wana nia mbaya kama vile kutaka kukudhuru kiakili au kimwili.

Hivyo basi, unapotumia intaneti, ni muhimu sana kuelewa na kufahamu fursa na hatari ambazo intaneti inaweza kukuletea. Kitini hiki kimetengenezwa ili kukujulisha na kukuongoza jinsi ya kufurahia na kuwa salama mtandaoni.

Natumaini kwamba utafurahia kitini hiki na utapata elimu ya jinsi ya kujilinda na udhalilishaji dhidi ya watoto mtandaoni. Daima, jihadhari na uwe salama mtandaoni.



Dkt. Zainab A.S Chaula
Katibu Mkuu

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum

TAFSIRI YA MANENO YALIYOTUMIKA KATIKA KITINI HIKI:

Arafa - Ujumbe mfupi wa maandishi

Dhuru - Kusababisha maumivu au majeraha ya mwili au akili au sifa za mtu kwa njia yoyote ile.

Dawati la Polisi la Jinsia na Watoto - Kitengo maalum ndani ya Jeshi la Polisi Tanzania chenye askari waliohitimu mafunzo maalum ya kushughulikia kesi za ukatili dhidi ya watoto na unyanyasaji wa kijinsia.

Intaneti- Mfumo unaunganisha ulimwengu kwa kusambaza na kupokea habari za kimaandishi, picha na video kielektroniki.

Mitandao ya kijamii - Programu tumizi za kompyuta zinazoruhusu watu kuwasiliana na kupeana taarifa kwenye mtandao kwa kutumia kifaa cha kielektroniki kama vile kompyuta au simu ya mkononi. Mfano wa mitandao ya kijamii ni Facebook, Twitter, Instagram na WhatsApp.

Kuposti - Kutuma ujumbe wa maneno, picha au video kwenye jukwaa la kielektroniki ili kuruhusu watu wengi kuuona.

Mawasiliano ya Kielektroniki - Nyenzo za habari ambazo ni za kielektroniki.

Mtandaoni - Kuingia kwenye mtandao kwa kutumia intaneti na kutumia huduma zake.


TEHAMA - Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Mchanganyiko wa teknolojia ya habari, utangazaji na mawasiliano.

Uraibu - Hali ya mazoea yaliyopitiliza katika kufanya kitu au utumiaji wa kitu flani ambao unaleta madhara kwa mtu kama kutumia intaneti kila mara.

Utambulisho - jina la mtu na taarifa ambazo zinamtambulisha.

UNAINGIAJE MTANDAONI? VIFAA VINAVYOTUMIKA KUKUUNGANISHA NA MTANDAO

Kabla hatujaanza safari yetu, Je, unaweza kutaja kila kifaa kinachotumika kukuunganisha kwenye intaneti hapa chini?



JE, UNAPENDA KUTUMIA PROGRAMU GANI KATI YA HIZI?



Rafiki yangu wa mtandao ameniomba nionane nae baadae!

Una uhakika unataka kwenda?



FAIDA NA FURSA ZA KUTUMIA MTANDAO

Mtandao una manufaa mengi. Zifuatazo ni baadhi ya faida ambazo unaweza kupata ukitumia mtandao:



Kujifunza mambo na ujuzi mpya



Kutazama video za kufurahisha na kusikiliza muziki



Kucheza michezo



Kuchangamana na marafiki



Kuwasiliana na marafiki na familia



Kuposti na kuonesha picha binafsi

KUWA MAKINI, KUNA UPANDE WA PILI WA MTANDAO: UHALIFU DHIDI YA MTOTO MTANDAONI!

Licha ya faida unazo weza kuzipata kupitia matumizi ya intaneti, unapaswa kuelewa kwamba mtandao unaweza pia kuwa hatari kwa watoto na vijana. Kuna hatari za aina nyingi dhidi ya watoto mtandaoni. Hatari hizi zina sura ya ukatili na unyanyasaji wa kingono kama ilivyoelezwa hapa chini.

Nyenzo za udhalilishaji watoto kingono.

Hizi ni picha, video, vitabu vya katuni, katuni na vingine vingi vinavyo onyesha sehemu za siri za mtoto au watoto wakinyanyaswa kingono.



Udhalilishaji na vitisho kwa kutumia picha.

Hii inamaanisha kulazimisha mtu kutuma picha na video chafu kisha kuzitumia dhidi yake. Mara nyingi waathirika wa hili hutishiwa kwamba wasipofanya ngono, kutoa pesa au kufanya mambo mengine na hao watu wanaotaka wafanye hivyo basi picha zao zitawekwa hadharani mtandaoni au kwenye mitando ya kijamii.

Kumrubuni mtoto mtandaoni.

Hii inamaanisha kujenga uhusiano na mtoto kupitia mtandao kwa lengo la kumdhalilisha kingono.




Meseji za Ngono. Hii inamaanisha kutuma au kupokea ujumbe wa maandishi, picha au video zenye maudhui ya kingono kutoka kwa watu wanaojulikana au wasiojulikana kwa lengo la kukushawishi kufanya ngono.

Udhalilishaji kingono mbashara. Hii ni pale mtoto anapolazimika kuchukuliwa video za ngono ama akiwa peke yake au na watu wengine. Wakati huo huo, video hii hupitishwa moja kwa moja mtandaoni na kutazamwa na wengine katika maeneo tofauti.



Uonevu mtandaoni ni pale mtu binafsi au kikundi cha watu kinapoamua kumwaibisha, kumfedhehesha, kumtishia, kumtusi au kumdhalilisha mtoto kupitia arafa za simu, mitandao ya kijamii au aina nyingine za mawasiliano ya kielektroniki. Hapa chini unaweza kupata baadhi ya mifano ya uonevu mtandaoni:

- Kutuma ujumbe mbaya au wa vitisho mtandaoni kuhusu mtoto.
- Kueneza uvumi mtandaoni ili kuharibu sifa ya mtoto mwingine.
- Kuiba akaunti ya mtandao ya mtoto mwingine na kuitumia kutuma ujumbe, picha au video za kuumiza.
- Kuunda akaunti mtandaoni ambazo zina hadithi, katuni, picha au vichekesho vinavyodhalilisha watoto wengine.
- Kupiga na kuweka picha ya aibu ya mtoto mwingine au rafiki mtandaoni.
- Kumdanganya mtoto mwingine au rafiki yako kwa lengo la kutoa habari zake binafsi na kuzisambaza kwa wengine.
- Kuchapisha taarifa za kuumiza au za uongo kuhusu mtoto au mtu mwingine mtandaoni.
- Kuhariri na kuweka picha za watoto wengine mtandaoni.



NANI ANAWEZA KUKUKATILI MTANDAONI?

Fahamu kuwa unaweza kufanyiwa ukatili mtandaoni na watu tofautitofauti ikiwa ni pamoja na wale unaowafahamu na usiowafahamu. Fahamu kwamba kuna watu unawafahamu lakini bado wanaweza kukudhuru. Hawa ni kama marafiki zako, jamaa, watu wa familia yako, wasichana wa nyumbani au wavulana wanaofanya kazi nyumbani kwako, walimu, na majirani.







Daima kumbuka kuwa mahasimu wa mtandaoni wanatumia utambulisho bandia ili kukufanya uamini kuwa wao ni watoto kama wewe, lakini mara nyingi hua sivyo.



NINI KITATOKEA NIKITUMIA MTANDAO MARA NYINGI?

Kutumia mtandao mara nyingi kunaweza kukufanya uepuke kukutana na marafiki na kupoteza hamu ya kufanya mambo unayopenda au mambo mengine ya kuvutia. Hali hii inaitwa uraibu wa mtandao. Ukiona baadhi ya hali zilizoorozeshwa hapo chini zinakutokea, basi jua unahitaji msaada.



-  Unapoanza kujisikia furaha zaidi ukiwa na marafiki mtandaoni na kuacha kukutana na marafiki nje ya mtandao.
-  Unapokua huwezi kujizuia kucheza michezo ya mtandaoni au kutumia mtandao bila lengo lolote.
-  Unapoanza kuepuka shule au shughuli za kila siku na kutumia muda mwingi mtandaoni.
-  Unapotumia muda mwingi wa siku yako mtandaoni.
-  Unapohisi hali ya huzuni, hasira unapoombwa kuacha kutumia mtandao.
-  Unapotumia mtandao ili ukufurahishe ukiwa na huzuni.

UNAWEZAJE KUBAKI SALAMA MTANDAONI?

Hapa kuna baadhi ya mambo muhimu unayoweza kuyafuata ambayo yatakuweka salama mtandaoni.


- Jua kwamba taarifa zako zinaposhirikiwa mtandaoni, huna udhibiti wala uwezo wa kuziondoa. Mara tu unapotuma au kuweka kitu mtandaoni unaweza kukifuta, lakini huwezi kukiondoa kabisa kwenye mtandao.
- Kamwe usipige au kuweka picha zako ama za mtu yeyote za faragha mtandaoni.
- Epuka kutoa taarifa zako binafsi na za familia yako kwa watu usiowajua na hata wale unaowajua. Taarifa hizi ni kama vile jina lako, eneo, anwani, barua pepe na nambari ya simu ya mkononi. Hizi zinaweza kutumika kwa urahisi kukutambua.
- Epuka kuweka picha zisizofaa, ikiwa ni pamoja na picha za ukatili wa kingono ama picha za ngono.
- Kamwe usimpatie mtu yeyote taarifa zako binafsi au za siri.
- Kuwa mwangalifu na unachoweka mtandaoni. Epuka kutoa taarifa zako kupita kiasi na kufichua mambo mengi ya maisha yako mtandaoni kwa sababu unachoweka mtandaoni kinaweza kutumika kama silaha ya kukuumiza.
- Kabla ya kuweka chochote mtandaoni, jiulize swali hili, "Je, hii ni sawa na wazazi wangu, jamaa, wanafamilia, walimu, Mchungaji/Imamu, Serikali au dunia nzima kuona ujumbe huo? Ikiwa sivyo, uhariri upya ujumbe au picha hio kabla ya kuweka mtandaoni.
- Hakikisha habari unaweka mtandaoni ni ya kweli na yenye heshima kwa watu wengine.
- Tunza nakala ya kila ujumbe usiofaa uliotumwa kwako kabla ya kuufuta. Hii inaweza kutumika kama ushahidi polisi au mahakamani.



WAPI UNaweza KUTOA TAARIFA?

Ikiwa mtu anakusumbua mtandaoni, au anataka ufanye mambo ambayo hutaki au anakutishia; chukua hatua na ufanye yafuatayo:

- Mwambie mama au baba yako au wanafamilia wengine unaowaamini; au
- Mwambie mwalimu unayemuamini, ikiwezekana mwalimu wa malezi, au ushauri nasaha na unasihi shuleni kwako; au
- Piga simu bila malipo kwa nambari ya msaada kwa watoto ambayo ni **116** ambapo unaweza kuzungumza na mtu na kupata usaidizi; au
- Tembelea Dawati la Jinsia na Watoto la Polisi na kuripoti suala hilo; au
- Tembelea dawati la ulinzi na usalama wa mtoto shuleni; au
- Tembelea Ofisi ya Ustawi wa Jamii iliyo karibu au piga simu ikiwa una nambari zao.



KABLA HATUJAMALIZA; JE, UNAJUA JINSI YA KUMBLOCK AU KUMZUIA MTU ASIONE TAARIFA ZAKO UNAPOWEKA MTANDAONI AU AMBAE HUTAKI KUWASILIANA NAE ASIKUSUMBUE?

Dondoo za kuwa salama wakati unatumia **Instagram**



- Zima taarifa inayohusiana na jiografia ya eneo ulipo kwa sababu sio salama kuonesha sehemu ulipo.
- Zima kitufe kinachoweza kuhusisha picha, video au taarifa za mtu mwingine kwenye kurasa yako au kushirikishwa kwenye taarifa ambazo hujaridhia.

Je unajua jinsi ya kuzuia mawasiliano yako na watu wengine?

1. Bonyeza jina la hio akaunti.
2. Bonyeza kitufe cha option chenye nukta tatu ... juu kulia
3. Bonyeza *block*. Hapo utakuwa umeshamzuia kuwasiliana naye.

Dondoo za kuwa salama wakati unatumia **Facebook**



- Kabla ya kuposti kitu chochote jiulize, je itakukera iwapo wengine wataisambaza? Kama ndio, ni vizuri usiiposti.
- Kabla hujamkubali mtu yoyote kuwa rafiki, jiulize mnafahamiana? Je kati ya marafiki zake kuna yoyote ambaye ni rafiki yako pia?
- Tafuta kitufe kilichoandikwa "*FIND SUPPORT OR REPORT POST*" kuwafahamisha Facebook kuhusu maudhui yenye kukera

UNAMFAHAMU ANAYEONA POSTI ZAKO?

1. Ingia kwenye facebook na bonyeza *menu*
2. Nenda kwenye "*PRIVACY SHORTCUT*"
3. Bonyeza *SEE MORE PRIVATE SETTING*
4. Bonyeza, "*WHO CAN SEE YOUR FUTURE POST*" halafu chagua.

Jinsi ya kuwa salama unapotumia **WhatsApp**



Kumbuka kuwa, mtu yeyote aliye na namba yako ya simu, anaweza kukutumia ujumbe katika WhatsApp.

- Kama utapokea ujumbe usiopendeza, fanya yafuatayo: fungua chat ya mtu huyo kisha gusa jina lililoko kwenye namba yake, halafu chagua na ubonyeze "*BLOCK*"
- Kama ulituma ujumbe kwa bahati mbaya, uchague halafu bonyeza "*DELETE*" halafu bonyeza *DELETE FOR EVERYONE*"

Kuzuia watu usiowajua kuona picha zako!

Tunashauri uruhusu picha ya WhatsApp *profile* kuonekana kwenye namba ulizonazo tu kwa kufanya yafuatayo:

1. Nenda kwenye "*SETTING*" halafu nenda kwenye "*PRIVACY*"
2. Halafu nenda kwenye "*PROFILE PHOTO*"
3. Mwisho chagua "*MY CONTACTS*" kwa maana wale unaowafahamu tu au "*NOBODY*" kwa maana ya wote wasione.

Jinsi ya kuwa salama unapotumia **YouTube**



1. Je, huwa unapakua video? Unapaswa kujua aina ya vitu unavyorekodi. Unayo taka kurekodi lazima yasiwe ya kikatili, ya hatari au ya kingono.
2. Tumia uchaguzi wa faragha wa YouTube kudhibiti ni nani anaweza kuona video unayoituma.
3. Kama kuna mtu amepakua video yako bila ridhaa yako, unaweza kuwaomba YouTube waondoe hiyo video kwa kuitolea taarifa.

UNAFAMU NAMNA YA KUITOLEA TARIFA VIDEO?

1. Bonyeza sehemu ya uchaguzi (*OPTIONS*) kwenye video unayotaka kuitolea taarifa.
2. Chagua "*REPORT*"
3. Chagua sababu ya kutoa taarifa kuhusu video hiyo.

Muhimu: Kumbuka mambo ya kingono yanayohusu watoto kwenye mtandao ni kosa kisheria na ni lazima uyatolee taarifa kwa mamlaka husika.

NATUMAI KUWA SASA UNAJUA JINSI YA KUFURAHIA MTANDAO NA KUWA SALAMA MTANDAONI KWA KUJILINDA NA KUWALINDA WENGINE.

unicef 

for every child